


**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA
TAASISI YA KUZUIA NA KUPAMBANA NA RUSHWA**



Barabara ya Kilimatinde Cheyo,
S.L.P. 1020,
45112
TABORA,
Barua Pepe: rbctabora@pccb.go.tz.
TANZANIA.
www.pccb.go.tz

TAARIFA KWA UMMA

TABORA, 13 OKTOBA 2020

**WATUMISHI WATANO WA HALMASHAURI YA
WILAYA YA SIKONGE KUFIKISHWA MAHAKAMANI**

Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa Mkoa wa Tabora tarehe 13/10/2020 inatarajia kuwafikisha Mahakamani watumishi watano (05) wa Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge kwa tuhuma ya kuomba na kupokea rushwa kwa wafugaji wa ng'ombe.

Watuhumiwa hao ni:

- Kelvin Evarist Msacky- Afisa wanyama pori Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge
- Lambert Emmanuel Kombo- Afisa misitu msaidizi Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge
- Manfred Dales Lyimo – Afisa misitu msaidizi Halmashauri ya Wilaya Sikonge
- Jovin Donat Sapola - Afisa misitu msaidizi Halmashauri ya Wilaya Sikonge na
- Edga Vedasto Rwezaura - Afisa misitu Mkuu Halmashauri ya Wilaya ya Sikonge

18,000,000/= toka kwa mfugaji waliyemkamata kwa madai kuwa alikuwa akilisha ng'ombe ndani ya hifadhi ya kijiji cha Kanala Wilaya ya Siikonge kinyume na kifungu cha 15 cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007.

Uchunguzi wa TAKUKURU mkoa wa Tabora umebaini pia kuwa watuhumiwa walitenda kosa hilo wakiwa katika zoezi la kuondoa mifugo kwenye hifadhi ya kijiji cha Kanala Wilaya ya Sikonge Mkoa wa Tabora.

Aidha, katika hatua nyingine mnamo tarehe 09/10/2020 TAKUKURU Mkoa wa Tabora iliwafikisha Mahakamani na kuwafungulia kesi ya jinai namba 91/2020 - Mashaka Mwang'oma Mfume – Mwalimu Mkuu Shule ya Msingi Chabutwa Wilaya ya Sikonge kwa kosa la kutoa rushwa ya Shs 80,000/= na Nyerembe Michael Kikudo - Mwalimu Shule ya Msingi Sikonge kwa kosa la kupokea rushwa ya Sh.80,000/= ili atoe nje ya chumba cha mtihani – karatasi ya mtihani wa sayansi ya darasa la saba uliokuwa ukiendelea. Kosa hili ni kinyume na kifungu cha 15(1) na (2) cha Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007

Washtakiwa hawa wote walipata dhamana na kesi itakuja kwa ajili ya kusomwa hoja za awali tarehe 03/11/2020.

Nitoe rai kwa watumishi wote wa mkoa wa Tabora ambao wameaminiwa na kupewa kazi wafanye kazi kwa kuzingatia uadilifu pasipo kujihusisha na rushwa.

Niwatake wote wanaojihusisha na rushwa ya aina yeyote ndani ya mkoa wa Tabora waache mara moja kwani TAKUKURU Mkoa wa Tabora tutawachukulia hatua kali za kisheria wale wote wanaojihusisha na vitendo vya rushwa.

Imeandaliwa na



Musa Chaulo

MKUU WA TAKUKURU MKOA